HALMASHAURI YA MJI HANDENI

SHULE YA SEKONDARI HANDENI

NAMBA ZA SIMU:

Mkuu wa Shule: 0717018235/0757094277
Makamu Mkuu wa Shule:0715204435

KUMB. Na.

Mwanafunzi……

……

S. L. P ……

…….

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA HANDENI KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

1.0. Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha Kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari ya Handeni ipo umbali wa Kilometa moja kutoka ofisi za Halmashauri ya Mji Handeni. Shule hii ni ya kutwa.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe ***11/01/2021.*** Unatakiwa kuripoti kuanzia tarehe ***11/01/2021*** saa moja kamili asubuhi na mwisho wa kuripoti ni tarehe ***25/01/2021.***

2.0.Mambo ya kuzingatia

2.1. Sare za Shule

(a) WAVULANA:

(i**) Suruali**: - Rangi ya kijivu yenye marinda mawili kila upande isiwe **inabana** (**upana chini iwe inchi 15)** na **iwe ndefu.**

(ii) **Shati:** - Jeupe mikono mifupi lisilobana,lenye kola na lisiwe fupi ili aweze kuchomekea kwa urahisi

(iii) **Sweta:-** Jeusi na linavaliwa kipindi cha baridi tu. **Majaket**i na **Makoti hayaruhusiwi kabisa**.

(iv) **Viatu**:Vyeusi vyenye kamba na visiwe na kisigino kirefu wala shingo ndefu wala vilivyochongoka, Soksi ni nyeusi, kahawia au bluu.

(v**) Mkanda-** Mweusi wa ngozi usiwe na bakozi kubwa na uwe na upana usiozidi inchi 11/2 au sentimita 31/2

(b) **WASICHANA**

(i) **Sketi** – Rangi ya kijivu yenye marinda ndefu inayovuka magoti kwa **inchi 4** au **sentimita 10.**

(ii) **Shati** – Jeupe la mikono mifupi lisilobana na refu linaloweza kuchomekewa kwa urahisi wale wanaovaa hijabu washone sketi ndefu inayoficha miguu na kuacha inchi 6 kutoka chini na iwe na marinda ya kawaida na shati la mikono mirefu lisilobana pamaoja na kitambaa kilichoshonwa kikubwa kisichobana.

(iii) **Viatu** – Vyeusi vyenye kamba visivyo na kisigino kirefu wala shingo ndefu wala vilivyochongoka Socks ni nyeupe.

(iv) **Sweta** – Jeusi na livaliwe wakati wa baridi tu. Majaketi hayaruhusiwi wala makoti

- Sare michezo: Fulana na Bukta kwa wavulana, Fulana, Bukta na Sketi kwa wasichana
- Sare za kazi za mikono: Watavaa T-shirt ya njano isiyo na maandishi pamoja na sketi au suruali ya Shule
- Raba za michezo ni rangi yoyote.

2.3 Mahitaji Mengine.

Mwanafunzi aje na vifaa vya kujifunzia kama ifuatavyo.

(a) Daftari zisizo pungua kumi (10).

(b) Kalamu za kutosha

(c) Mkebe wa mahesabu (Mathematical set)

3.0 Sheria,Kanuni na Taratibu Muhimu za Shule

3.1 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria namba 26 ya mwaka 1970. Aidha inazingatia miongozo yote ya Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi;

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.

(c) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.

(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.

(f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(h) Mwanafunzi atakapofika shuleni awe amekata nywele na ziwe fupi njiti ya kiberiti isiweze kukaa na zisiwe zimewekwa dawa. Shuleni hakuna kusuka nywele.

(i) Kucha ziwe fupi na zisiwe zimepakwa rangi au hina.

3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, Cocaine, mirungi, kubeli n. k.
5. Kupiga au kupigana
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

7. Kudharau bendera ya Taifa
8. Kuoa au kuolewa
9. Kupata mimba, kutoa mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
10. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
11. Kukataa adhabu kwa makusudi.
12. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi shuleni.
13. Kutokuhudhuria darasani pasipo sababu ya msingi.

4.0 Mambo mengine muhimu

(a) Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(c) Fomu ya Mzazi/Mlezi kukiri kukubaliana na sheria na kanuni za shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

"KARIBU SANA HANDENI SEKONDARI"

……
LUSUBILO S. SICHONE
MKUU WA SHULE

HANDENI SECONDARY SCHOOL
MEDICAL EXAMINATION FORM

(A): REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

MEDICAL OFFICER,
GOVN. HOSPITAL,
……..
…….

NAME OF PUPIL……..
Please examine the above named girl/boy to ascertain her/his fitness for further studies.

……..
HEADMASTER

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by the medical officer)
I have examined the above named with regard to:
Skin…….
Eyes…….
Ears……..
Chest…….
Spleen……...
Abdomen……..
Urine…….
Stool…….
Hemoglobin…….....
Pregnancy Test ……..

And I considered:

1. She/he is good health, free from infection diseases, worms, bilharzias and fit to go to school.
2. She/he is now fit to return to school having treatment for……..
   ……
   …….

…… …….
NAME AND SIGNATURE OF MEDICAL OFFICER DATE